# KUMWONA YESU NA MATENDO YAKE MAKUU KUNAHITAJI JUHUDI BINAFSI (JITIHADA BINAFSI)

## Maandiko: Luk 19: 1 – 10

1. **UTANGULIZI**

   Kama kuna siri ya ajabu ambayo nimeigundua ndani ya maisha haya ya wokovu, ni siri ya jitihada binafsi katika kufikia malengo fulani uliyojiwekea. Jitihada binafsi hata kwa mwanafunzi anayesoma ndizo zitakazomfanya afahamu mengi na kufaulu sana tofauti na wenzake; jitihada binafsi hata kwa mfanyabiashara ndizo zitakazomtofautisha na wafanyabiashara wenzake baada ya muda mfupi; yaani jitihada binafsi kama unataka kufika mahala fulani katika maisha haya ni za muhimu sana. ***2Timoth 2: 15.***

- Katika kisa hiki tunamwona Zakayo mtu mfupi kuliko watu wote anafanya jitihada binafsi za kupanda juu ya mkuyu (awe juu ya wote) kwa lengo la kumwona Yesu. **Jitihada za Zakayo zilimgusa sana Yesu hadi akabadili ratiba yake ya siku hiyo yote; akaamua ashinde na mtu mmoja ambaye ana hamu kubwa naye kuliko kuongozana na wapambetu tu.**

**Note**: **Hamu ndani ya mtu wa Mungu ya kutaka kuona mabadiliko katika maisha yake humsukuma kuwa na juhudi/ jitihada binafsi za kuomba na kusoma neno la Mungu daima mpaka mbingu zinashindwa kunyamaza kwa ajili ya mtu huyo!!** Haikuwa rahisi Yesu akashinde ndani ya nyumba ya Zakayo aliyekuwa na sifa mbaya katika jamii na ambaye jamii iliwa haimpendi kutokana na maisha yake ya dhuluma na kubambikizia watu kodi kubwa na kupokea rushwa.

- **Yesu alipoona jitihada binafsi alizochukua Zakayo – Ofisa Mkuu wa TRA akapande juu ya mti kama wahuni wafanyavyo kwa lengo tu la kumwona Yesu ni mtu wa namna gani. Jambo hili lilimgusa sana Yesu anayeona haja zetu tangu mwanzo.** ***Yoh 1: 47 – 50.***

2. Mifano ya watu ambao jitihada zao binafsi zilisababisha miujiza yao kutokea.

(a)***Mark 10: 46 – 52.*** Bila jitihada binafsi hapa, muujiza wa Bathoromayo kuona ulishazibwa na watu wanaomzunguka Yesu. Hakukubali wanadamu wamnyamazishe; alijitosa kweli kweli hadi Yesu akasikia na kumwita.

(b) ***2Wafalme 4: 18 – 37*** - Jitihada za mwanamke huyu sio za Kawaida; alifikia hatua ya kung'ang'ania mguu wa nabii na hakuna mtu anayeweza kabisa kumtoa!! ***Mst 27 – 28!!*** Jitihada hizi zikamfanya nabii aahirishe mambo mengine yote na kwenda naye na matokeo yake ni mtoto wake kufufuka. Heleluya.

***(c)Mark 5: 25 – 34.*** Ukitaka kufahamu kwa kina juhudi binafsi za huyu mwanamke aliyeponywa, soma kwanza desturi ya Wayahudi ambayo mwanamke alikuwa hachangamani na wanaume!! Na hata mkutano huu mkubwa wa Yesu; waliokuwa wanamsongasonga Yesu ni wanaume; lakini huyu mwanamke **akajitosa** maadamu ameweka azimio ndani ya moyo wake (alisema moyoni mwake (maana yake aliazimia) liwalo na liwe lakini naenda!!

"**Ndugu zangu Yesu na matendo yake makubwa siyo ya mkumbo; ni ya yule anayejitahidi!! Hata mbinguni watakaoingia, ni wale waliojitahidi kupambana na dudu hili dunia; dudu hili mwili pamoja na dudu hili shetani. *Luk 13: 22 – 24.* Soma kwa makini maneno haya ya Bwana Yesu!! *Math 11: 12***

***(d)Luk 5: 17 – 26.*** Kama kuna jitihada binafsi zilizofanyika ili huyu mgonjwa aliyepooza apate kufika mbele za Yesu, hizi ni kiboko yake. ***Marko 2: 1 – 12* yeye anasema walitoboa dari ya nyumba ya mtu ili mgonjwa wao apite!!** Yesu akaona jitihada kama hizi, anashindwa kujizuia asitende muujiza!! Na katika kutenda muujiza huu, Yesu anaagiza, jitwike kitanda chako!! Au inuka n.k yaani fanya juhudi, chukua hatua!!

(e) ***Mwanzo 32: 24 – 30.*** Jitihada za Yakobo usiku kucha anapambana ili Malaika wa Bwana ambariki!! Hadi anateguka uvungu wa paja lakini hamwachi hadi alipopata ushindi!! Kubadilishwa jina toka Yakobo (mwongo, lagai na kuwa Israel yaani Mbarikiwa haikuwa jambo jepesi!! Tangu siku hii Israeli aligeuzwa na kuwa mtu mwingine kabisa na mpaka mwisho wa maisha yake unakuwa wa ajabu. ***Mwanzo 49: 33 *29 – 33*** akafahamu hata wakati wa kufa kwake, akatoa maelekezo kwa watoto wake, lakini kwanza akawabarikia kila mmoja. Yakobo ndiye aliyezaa makabila **12** yanayounda Taifa la Israel hadi leo.

(f) ***1Samwl 1: 9 – 20.*** Hana alichukua jitihada binafsi katika kutatua tatizo alilokuwa nalo; alitupilia mbali faraja za wanadamu, akaweka kando uzuri wake kama alivyofanya Zakayo na usiku ule ule Bwana akamtokea; na historia yake ikabadilishwa kabisa. ***1Samwl 2: 1 – 11***

3. Mwaka **2021** siyo wa kutembea **kimkumbomkumbo;** mafanikio na baraka za kila mtu wa Mungu ziwe za kiroho au za kimwili zinategemea juhudi binafsi za kila mmoja wetu katika kumtafuta Mungu na katika kuchapa kazi; Rais hataleta maendeleo na mafanikio yagu ng'oo!! Hatima yangu ninayo mimi mwenyewe ya sasa na ya milele. ***1Nyak 4: 9 – 10.*** Ukiwa na maswali kama haya "nitakaa katika hali hii hata lini?" ***2Wafal 7: 3 – 11 *3 – 4,* Hata toba ya kweli inahitaji juhudi binafsi, jitihada binafsi ndicho kitu anachokiangalia sana Yesu kuliko kuvizia toba ya mkumbo!! *Luka 15: 14 – 24 *17 – 20.***

***Note:*** **Mafanikio yangu yote, Mungu ameyaweka ndani yangu mwenyewe.** "Yesu anawathamini sana wale wote walio na juhudi binafsi ambao hawakubali kamwe kukatishwa tamaa na watu wengine au mazingira, na kwa vyovyote vile wale wote walio na jitihada binafsi za kumtaka Bwana na Baraka zake pamoja na nguvu zake 2021 watamwona. ***Math 15: 21 – 28.*** Amina

***Na***
***Askofu Dr. L. Mwizarubi***
***10/01/2021***